MUDA: SAA 2.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION AND CULTURE
FORM TWO SECONDARY EDUCATION EXAMINATION, 1991

0011 ELIMU YA SIASA

MUDA: Saa 2

Jibu maswali YOTE katika karatasi hii na andika namba yako ya mtihani kila ukurasa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU

SWALI	ALAMA	SAHIHI
1		
2		
3		
4		
5		
6		
JUMLA		

Karatasi hii ina kurasa 8 zenye maandishi.

1. Katika swali hili lenye vipengele (i) - (xx) kuna majibu manne kwa kila kipengele. Chagua jibu lililo sahihi kwa kila kipengele na kuandika herufi inayostahili katika kisanduku kilichoko kando ya kila kipengele.

Mfano: Utaratibu wa maisha ya mwanzo wa maendeleo ya binadamu

A. Ukabaila
B. Utumwa
C. Ujima
D. Ubepari

C

(i) Wazo la uhuru lilikuwepo

A. wakati TANU ilipozaliwa
B. muda mfupi kabla ya Waingereza kututawala
C. kwa ajali tu katika mawazo ya wananchi
D. tangu hapo wageni walipoanza kuivamia nchi yetu.

(ii) Mwongozo wa Chama cha TANU wa 1971 ulikuwa na lengo la

A. kulinda, kuimarisha na kuendeleza mapinduzi ya Tanzania na Afrika.
B. kulinda haki na shughuli za kiushirika na za kijamaa nchini
C. kuwapa wananchi madaraka na uwezo zaidi wa kujipangia maendeleo yao.
D. kutambuliwa na kupewa haki wananchi waliojumuika pamoja vijijini.

(iii) Msingi mkubwa uliofanikisha Muungano wa Vyama vya TANU na ASP ni:-

A. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
B. Uhusiano wa kihistoria uliokuwepo tangu kuanzishwa kwa vyama hivyo.
C. Kuwepo kwa serikali mbili
D. Mapinduzi ya 1964 huko Visiwani.

(iv) Elimu ya Kujitegemea ni

A. elimu ya kujiendeleza mashuleni katika kujitegemea kwa kutumia kilimo.
B. malezi ya Taifa la Tanzania kuwezesha wakulima na wafanyakazi kujikomboa kisiasa, kiutumaduni na kiuchumi
C. kujitegemea kwa kutumia elimu ya Tanzania ili kujenga taifa lililo sawa na huru
D. elimu mahsusi ya nadharia.

(v) Mfumo wa ujima haukuwa wa kinyonyaji kwa sababu

A. wote walikuwa matajiri
B. bidhaa zilikuwa haziadimiki
C. kazi ilikuwa kwa wote wenye uwezo
D. fedha ziligawanywa sawa.

(iv) [illegible]

A. Waremp
B. Waingereza ( )
C. Wajerumani
D. Waarabu

(vi) katiba yetu ya serikali ya Muungano imezingatia sana

A. usawa, upendo ujamaa na haki
B. udugu, ukweli, ujamaa na uhuru
C. umoja, ujamaa, sheria na uongozi
D. uhuru, haki, udugu na amani.

(vii) Mwalimu J.K. Nyerere alitoa pendekezo kuunganishwa vyama vya TANU na ASP ili

A. awepo Rais wa nchi peke yake na Mwenyekiti wa Chama peke yake
B. achaguliwe kuwa mwenyekiti wa CCM
C. kuwa na chama kimoja cha kudai uhuru
D. kiwepo chama kimoja cha siasa katika Tanzania.

(viii) Uchaguzi Mkuu unaweza kufanyika endapo:

A. Bunge litavunjwa rasmi baada ya muda wake wa miaka mitano
B. Wabunge wataamua uchaguzi mkuu ufanyike
C. Kamati kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itaamua uchaguzi ufanyike
D. Ikiwa baadhi ya mambo katika katiba yatabadilika.

(ix) Wenye uwezo wa kubuni, kujadili, kuamua na kutoa miongozo ya siasa ya Chama ni

A. Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa
B. Halmashauri Kuu ya Taifa
C. Sekretarieti ya Siasa
D. Mkutano Mkuu wa Taifa

(x) Shabaha ya kwanza ya TANU ilikuwa ni

A. Kuipinga TAA
B. Kueneza Siasa ya Ujamaa
C. Kuikomboa Tanganyika
D. Kupinga serikali ya Mseto

(xi) A.S.P. ni Muungano wa vyama vya

A. Z.P.P., A.N.C. na Z.N.P.
B. Shirazi Association na Arab Association
C. Shirazi Association na African Association
D. Z.P.P. na Z.N.P.

(xii) Chama kilichodai hali bora za maisha hasa kwa watumishi wa serikali wananchi (Tanganyika) ni

A. African Association
B. Tanganyika African Association
C. Tanganyika African National Union
D. African National Congress

Candidate's Number _____

(xiii) Ujima, Utumwa, ukabaila, ubepari na ujamaa ni
A. mifumo ya jamii ya kinyonyaji
B. utaratibu wa maisha ya jamii
C. maneno yanayotumiwa na wanasiasa
D. mifumo inayozingatia usawa wa binadamu.

(xiv) Mahakama ya Rufaa ni
A. Mahakama ya Muungano inayosikiliza kesi za rufaa.
B. Mahakama inayoongozwa na Jaji Kiongozi
C. Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano
D. Mahakama maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

(xv) Ifuatayo siyo kazi ya Bunge la Muungano.
A. Kutunga sheria
B. Kuteua serikali kwa kila hali
C. Kutoa malengo ya muda mrefu na muda mfupi
D. Kuteua viongozi wa Chama na serikali katika ngazi za mikoa na wilaya.

(xvi) Vita vya Maji Maji dhidi ya Wajerumani vilipiganwa kwa sababu:
A. Waafrika walikuwa wamekunywa dawa ya maji
B. Wangoni walipinga kulima pamba
C. Wananchi walitaka kuondoa uonevu na udhalimu wa kikoloni.
D. Kinjeketile Ngwale alianzisha vita hivyo.

(xvii) Kipi kati ya vifuatavyo kwa mujibu wa Katiba ya CCM ni Kamati ya Mkutano Mkuu wa Taifa?
A. Bunge
B. Tume ya Tabia ya Viongozi
C. Muungano wa madiwani wote nchini
D. Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu.

(xviii) Ubeberu katika Afrika ulisababishwa na
A. Ukoloni mamboleo
B. mapinduzi ya viwanda na maendeleo ya Ulaya
C. safari za Wamisionari na Wapelelezi
D. mfumo wa ukabaila

(xix) Kila tarehe 5 Februari tunasherehekea sikukuu tatu ambazo ni
A. Kuzaliwa kwa ASP, CCM na Azimio la Arusha
B. Kuzaliwa kwa ASP, TANU na Azimio la Arusha
C. Kuzaliwa kwa Azimio la Arusha, CCM na TANU
D. Mapinduzi, Muungano na kuzaliwa kwa A.S.P.

D. Ukabaila

(i) Zipi kati ya sentenso zifuatazo zinaelezea kwamba kuu tatu za maisha ya ujima kushi pamoja.

5 - Candidate's Number _____

(xx) Nia ya Watanganyika kuanzisha vyama vya wakulima na wafanyakazi wakati wa ukoloni ilikuwa

A. kuhamasisha wakulima na wafanyakazi ili wote wazalishe mali kwa bidii
B. kuwapendeza wakoloni
C. kupata njia ya mawasiliano kati ya wakulima na wafanyakazi
D. kupigana na unyonyaji, uonevu, ukoloni na hali zote za unyanyasaji zilizomkabili Mwafrika.

2. Kwenye nafasi ulizopewa baada ya kila tamshi andika "K" iwapo tamshih hilo ni kweli na "S" iwapo siyo kweli.

Mfano: Azimio la Musoma linahimiza elimu ya sekondari kwa wote S

(a) Chama cha ASP kilinyimwa ushindi katika uchaguzi wa 1963 kwa sababu ya hila za utawala wa Kiingereza _____

(b) "Binadamu wote ni sawa" maana yake binadamu ana akili kuliko mnyama _____

(c) Utumwa ni utaratibu wa maisha wa mwanzo kabisa wa kinyonyaji _____

(d) Siasa ya ndani ya Tanzania ni ya kutofungamana na upande wowote _____

(e) Makatibu wa CCM ni viongozi wa kuteuliwa _____

(f) Vyama vya demokrasia jamii huamini baadhi ya mambo ya kijamaa na kibepari _____

(g) Vita vya awali kabisa vya ukombizi nchini vilikuwa vile vya Maji Maji _____

(h) Kuwepo kwa serikali ya chama kimoja kunawanyima wananchi uhuru wa kutoa maoni yao _____

(i) Hali ya nchi moja kutawaliwa na nchi nyingie kisirisiri hasa kiuchumi huitwa ukoloni _____

(j) Katibu wa Chama wa Mkoa huchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama wa Mkoa _____

3. Oanisha vifungu cya maneno vya Kundi A na vile vya Kundi B ili vilete maana inayokusudiwa kwa kuandika namba za kundi B kwenye nafasi zilizowekwa kwenye Kundi A.

KUNDI A

(a) Ni mahakama ya mwisho katika Tanzania ( )
(b) Inashughulikia masuala yoyote ya kupanga na kusimamia Uchaguzi ( )
(c) Mwakilishi wa Serikali Bungeni ( )
(d) Kilimo ( )
(e) Azimio la Musoma ( )

(f) Ubepari uliokomaa ambao huvuka mipaka nje ya nchi yake ( )

(g) Chombo cha utekelezaji wa maagizo ya chama ( )

(h) Umoja wa watu wenye nia moja ya kutaka kushika au kudumisha madaraka ya Uongozi wa nchi. ( )

KUNDI B

1. Serikali
2. Tamko la Chama linalohusu siasa ya Ujamaa na Kujitegemea
3. Ukoloni Mamboleo
4. Ufashisti
5. Mahakama Kuu
6. Tume ya uchaguzi
7. Uti wa mgongo wa Uchumi wa Tanzania
8. Spika wa Bunge
9. Mahakama ya Rufaa
10. Tume ya Uchunguzi
11. Utekelezajiwa Elimu ya Kujitegemea
12. Chama cha Siasa
13. Waziri Mkuu
14. Katiba
15. Bunge.

4. Jaza majibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi

(a) Maana halisi ya Azimio la Arusha ni _____

_____

_____

(b) Mambo manne yaliyo chini ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(iv) _____

(c) Njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba demokrasi inafuatwa na kudumishwa katika chama ni-

_____

_____

_____

(d) Kazi mbili za Baraza la Mawaziri Tanzania ni:-

(i) _____

(ii) _____

(e) Vyombo vitatu vya utekelezaji wa siasa ya CCM ni:-

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(iv) _____

(f) Tume zinazohakikisha kuwa viongozi na vyombo vya utekelezaji vinaheshimu haki za wananchi ni:-

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(g) Moja ya madhumuni ya kuanzishwa kwa madaraka mikoani ilikuwa ni

_____

_____

(h) Lengo moja la elimu iliyotolewa wakati wa ukoloni wa Kiingereza hapa nchini ni _____

_____

(i) Wanachama waasisi wa CCM ni wale ambao _____

_____

5. Kamilisha habari ifuatayo kwa kujaza sehemu zilizoachwa wazi.

Wakoloni walitanguliwa na wafanyabiashara (i) _____ na wapelelezi. Walipokuja katika Bara la Afrika walikuwa na madhumini mbalimbali kwa kutafuta malighali kwa ajili ya (ii) _____ vyao huko Ulaya. Pili kutafuta (iii) _____ au mahali pa kuuzia bidhaa zao; na tatu kutafuta (iv) _____ ambako wangeweza kutawala watu (v) _____ (vi) _____ (vii) _____ (viii) _____

Kuja kwa wakoloni kumesababisha bara letu (ix) _____

vipande vipande. Mkutano wa kuligawa bara letu ulifanyika mwaka (x) _____ huko Berlin Ujerumani.

6. Eleza kwa kifupi maana ya dhana zifuatazo

(a) Utawala msonge _____

_____

(b) Uwangi meza _____

_____

(c) Ubwanyenye _____

_____

(d) Ubeberu _____

_____

_____

_____